HALMASHAURI YA MJI NEWALA

BARUA ZOTE ZLANDIKWE KWA MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI NEWALA

Simu Na: (+255) 023 2410673

Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P 39,
NEWALA

Unapojibutafadhalitaja

Kumb.Na.NTC/I.20/05/132 13/02/2020

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI (LINARUDIWA)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Newala anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI (1)

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Mwombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashada Cheti "NTA Level 5" katika fani zifuatazo:- Utawala,Sheria,Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI:-

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia/Sera, Sheria na Taratibu katika Kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.

- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.

MSHAHARA:-

- Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina Mshahara wa TGS B kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA:-

i. Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
ii. Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
iii. Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishe barua yake ya maombi kwa Mwajiri wake.
iv. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
vi. "Testmonials" Provisional results",Statement of results" nk hazitakubalika.
vii. Waombaji waweke picha moja ya" passport size" katika barua zao za maombi.
viii. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA.
ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 26/02/2020 saa 9.30 alasiri
x. Barua zote zitumwe kwa anuani iliyopo hapa chini.

MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P. 39,
NEWALA.

NB:- Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Mji Newala ambayo ni info@newalatc.go.tz

Andrew Frank Mgaya,,
MKURUGENZI WA MJI,
NEWALA.

Nakala:- Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa umma,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 63100,
11404 DAR ES SALAAM.

" Tovuti ya Halmashauri,
www.newalatc.go.tz

" Mbao za Mtangazo